

e-GA Yaanika Mikakati Kutekeleza Dira 2050, Yajivunia Mafanikio

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imeanika mikakati yake ya kutekeleza malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, yanayolenga asilimia 80 ya huduma za Serikali zipatikane kupitia mifumo ya kidigitali iliyo salama na jumuishi.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni kuimarisha usimamizi wa mtandao wa mawasiliano ya Serikali pamoja na mifumo ya TEHAMA, ili kupunguza urudufu wa mifumo na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Benedict Ndomba ameyasema hayo Februari 17, 2026 katika Kikao Kazi cha Sita cha Serikali Mtandao kilichofanyika Februari 17, 2026 jijini Arusha.

Kauli mbiu ya Kikao kazi hicho kilichohudhuriwa na wadau zaidi ya 1400 ni "Kuboresha utendaji kazi wa Serikali kwa Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Umma Kupitia Mifumo Salama na Jumuishi ya Serikali Mtandao".

Mhandisi Ndomba amesema, hatua hizo zinawezesha Serikali kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa kati ya taasisi mbalimbali za umma, jambo linaloongeza

kasi ya utoaji huduma na kupunguza gharama za uendeshaji wa mifumo ya TEHAMA Serikalini.

Ameeleza kuwa, utekelezaji wa mikakati hiyo unaendana pia na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2025, inayolenga kuhakikisha zaidi ya asilimia 50 ya huduma za Serikali zinapatikana kidigitali ifikapo mwaka 2030.

Kwa upande wa mafanikio ya kimataifa, amesema utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao umeiwezesha Tanzania kutambulika katika majukwaa mbalimbali, ikiwemo kupata tuzo za ubunifu katika huduma za umma kutoka Umoja wa Mataifa Mwaka 2024 na 2025 kupata tuzo ya 'World Summit on the Information Society - WSIS' kupitia mfumo wa e-Mrejesho toleo la pili, uliosaidia kuimarisha ushiriki wa wananchi katika utoaji wa maoni na maboresho ya huduma za Serikali.

Aidha, amesema Ripoti ya mwaka 2025 ya Benki ya Dunia kuhusu ukomavu wa matumizi ya teknolojia jumuishi katika utoaji wa huduma za Serikali, imeiorodhesha Tanzania katika kundi A la nchi zenye ukomavu wa juu wa matumizi ya TEHAMA, hatua inayoonesha mafanikio ya mageuzi ya kidigitali Serikalini.

"Mwaka 2022 Tanzania pia ilitajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazofanya vizuri zaidi katika eneo hilo na kushika nafasi ya pili barani Afrika. Nimshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada zake za kuwezesha sekta ya TEHAMA na mageuzi ya kidigitali, sambamba na kuiwezesha Mamlaka kutekeleza majukumu yake," amesema.

Ameongeza " Kauli mbiu ya mwaka huu inaakisi dhamira ya Serikali ya kutumia mifumo ya kidigitali iliyo salama na jumuishi ili kuongeza tija, ufanisi na uwajibikaji katika utendaji kazi pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi."

Hata hivyo, ametaja changamoto zinazokabili utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kuwa ni pamoja na upungufu wa wataalam wabobezi wa TEHAMA, mabadiliko ya haraka ya teknolojia yanayohitaji mafunzo ya mara kwa mara, kwa watumishi, pamoja na umuhimu wa taasisi kuimarisha usimamizi wa miradi ya TEHAMA ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhandisi Ndomba amesema jumla ya wadhamini 44, wamedhamini kikao kazi hicho, ambapo kati yao 10 ndio wadhamini wakuu, ambao ni Taasisi ya Moyo ya

Jakaya Kikwete – JKCI, Yas Mix By Yas, SoftNet, Info Gear, Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Vodacom, Bodi ya Sukari, Benki ya NMB na SOPHOS.

Kwa pande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ), Dkt. Said Seif Said, amesema wamekuwa wakishirikiana kwa kiwango kikubwa na e-GA katika kupiga hatua ya mageuzi ya kidigitali.

